

USHAHIDI WA UFUFUO



[Ndugu Orman Neville anasoma Luka 24:1-32—Mh.]

[Hata siku ya kwanza ya juma, ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakileta manukato waliyoweka tayari, na wengine pamoja nao.]

[Wakalikuta lile jiwe limeviringishwa mbali na kaburi.]

[Wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu.]

[Ikawa, walipokuwa wakifadhaika kwa ajili ya neno hilo, tazama, watu wawili walisimama karibu nao, waliovaa nguo za kumetameta:]

[Nao walipoingiwa na hofu, na kuinama kifudifudi hata nchi, hao waliwaambia, Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu?]

[Hayupo hapa, amefufuka: kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa akaliko Galilaya,]

[Akisema, Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa watu wenye dhambi, na kusulubiwa, na kufufuka siku ya tatu.]

[Nao wakayakumbuka maneno yake,]

[Wakaondoka kaburini, wakawaarifu mambo hayo yote wale kumi na mmoja, na wengine wote.]

[Nao ni Mariamu Magdalene, na Yoana, na Mariamu mamaye Yakobo, na wale wanawake wengine waliokuwa pamoja nao, hao waliwaambia mitume habari ya mambo hayo.]

[Maneno yao yakaonekana kuwa kama upuuzi kwao, wala hawakusadiki.]

[Lakini Petro aliondoka, akaenda mbio hata kaburini; akainama akachungulia ndani, akaviona vile vitambaa vya sanda tu vimewekwa peke yake, akaenda zake akiyastaajabia yaliyotukia.]

[Na tazama, siku iyo hiyo watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo wa saa mbili.]

[Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yote yaliyotukia.]

[Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaambatana nao.]

[Lakini macho yao yakafumbwa wasimtambue.]

[Akawaambia, Ni maneno gani haya mnyosemezana hivi mnapotembea, na huku mna huzuni?]

[Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je, wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yalipotukia huku siku hizi?]

[Akawauliza, Mambo gani? Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote:]

[Tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulubisha.]

[Lakini sisi tulitumaini kwamba yeye ndiye atakayewakomboa Israeli: na zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo haya.]

[Naam, tena wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushtusha, waliokwenda kaburini asubuhi na mapema;]

[Wasiuone mwili wake, wakaja wakisema ya kwamba wameona maono ya malaika waliosema yu hai.]

[Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini, wakaona vivyo hivyo kama wale wanawake walivyosema, ila hawakumwona.]

[Ndipo akawaambia, Enyi msiofahamu, na wenye mioyo mizito kuamini yote walivyoyasema manabii:]

[Je, haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?]

[Na kuanzia Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.]

[Wakakikaribia kile kijiji walichokuwa wakienda: naye akafanya kana kwamba anataka kuendelea mbele.]

[Lakini wakamshawishi wakisema, Kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa pamoja nao.]

[Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa.]

[Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao.]

[Wakaambiana, Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?]

³ Imekuwa siku nzuri sana kwangu, leo hii. Imekuwa nzuri sana kwa njia nyingi. Bila shaka, nimekuwa na umri mkubwa zaidi kidogo, leo, kwa hiyo inaifanya kuwa nzuri zaidi, na ninazidi kuwa na umri mkubwa zaidi. Lakini mimi... Imekuwa siku nzuri sana kwa sababu ni Pasaka. Na, basi, siku kuu kwa sababu jambo fulani limenipata siku hii, ambalo ninalo, sitalisahau kamwe. Ilikuwa ni shauku iliyokuja moyoni mwangu. Kwamba mimi...

⁴ Maishani mwangu mwote nimekuwa nikishangaa juu ya mambo, na kwa nini nilizaliwa katika ulimwengu huu.

⁵ Ndipo nilikuwa nikiwazia tu, asubuhi ya leo, nilipokuwa nikizungumza juu ya Musa. Na, yeye, ni nini hapana shaka kilikuja niani mwake alipogundua kwamba yeye alikuwa Mwebrania! Kwa nini Mungu amruhusu kulelewa katika ikulu ya Farao, na kisha kuchukua mahali, mahali huko nyuma ya jangwa, apate kujua kile alichopaswa kufanya maishani?

⁶ Na mara nyingi nimeshangaa, nikiwa mvulana, jinsi ambavyo Mungu, katika siku za mwanzoni, alikuwa akizungumza nami. Kisha nashangaa kwa nini aliruhusu picha hiyo kupigwa. Nashangaa kwa nini alifanya hivyo Ujerumani na Ufini. Nashangaa mbona mambo haya yote yametukia. Kamwe siwezi kuamini ilikuwa ni kwa sababu kwamba... Maana, mimi si mhubiri; sina elimu. Sina uwezo wa kuwa mhubiri. Ni lazima iwe ni kitu tofauti. Ninaamini watu wa Mungu wako utumwani. Ninaamini wako utumwani kwa sababu ya mapokeo ya mwanadamu. Na, siku hizi, tuna makumi ya maelfu wanaokufa kila siku, kwa magonjwa ambayo sayansi ya matibabu haiwezi kugusa, nao ni watoto wa Mungu. Nami ninaamini... hu—huenda nisiishi kuiona. Lakini ninaamini ya kwamba saa inakuja, na hiyo inaweza kuwa karibu, ambapo Mungu atafanya jambo kwa njia hii, kuthibitisha ya kwamba Yeye angali ni Mwenyezi Mungu. Na—naamini hilo. Nimeliona, kwa kipimo, lakini naamini ilikuwa kipimo kidogo kwa kile tutakachokiona.

Sasa, nitaondoka, asubuhi, kwa kipindi cha kupumzika kidogo.

⁷ Ambapo, mimi, leo, mimi katika maji hayo... Nilibatiza, mara nyingi, lakini nilipata baridi zaidi leo kuliko nilivyowahi kupata maishani mwangu. Nilipata baridi sana hata niliongea kwa shida. Ilikuwa tu kwa sababu ya “kudhoofika.” Nimekuwa njiani tangu Krismasi, au mara tu baada ya Krismasi, pasipo na angalau usiku wa mapumziko. Wala sina homa mbaya, lakini mimi ni dhaifu tu na nimedhoofika.

⁸ Ninashuka ziwani, kesho, Bwana akipenda, kuchukua siku chache za kupumzika. Nitarudi, Bwana akipenda, katika siku chache. Nasi tutakutana pamoja tena, kabla sijaenda kwenye

ibada, Mungu akipenda, ambayo ni kama siku kumi tu, kama siku ishirini kutoka sasa.

⁹ Kisha narudi, mwezi mzima, katika majimbo ya New England. Nirudi. . .Huo ni mwezi mzima wa Mei, kukiweko na siku mbili, siku mbili au tatu za mapumziko.

¹⁰ Kisha kutoka hapo, sina zaidi, angalau siku tano, kabla sijaenda Afrika. Hayo yote ni kwenye mwezi wa Juni.

¹¹ Na itakuwa ngumu. Nitalitegemea kanisa hili dogo, watu hawa, wakiniombea; kwa maana ninayahitaji, nayahitaji sana sana.

¹² Na, mnajua, hakuna mtu atakayejua, upande huu wa Utukufu, jinsi yote yamekuwa, na mapambano ambayo nimelazimika kupitia. Siwaambii watu. Hakuna haja ya kuwaambia watu. Wasingeweza kuelewa. Wala mimi sielewi. Ni kitu tu, unaendelea tu, kusonga mbele tu.

¹³ Sasa, ili watu wanaosimama wasilazimike kusimama kwa muda mrefu sana, nimechagua kwa ajili ya somo, usiku wa leo, somo hili, kama vile Ndugu Neville alivyosoma hivi punde Luka 24, kuhusu ufufuo. Somo langu usiku wa leo ni: *Ushahidi Wa Ufufuo*. Na sasa, alipokuwa akisoma, kulikuwa na mambo kadhaa ambayo Yeye alizungumzia, hapa, ambayo ningetaka kuyarejelea. Na hayo ni, la kwanza, kwamba hawa waliokwenda kaburini, kwanza, asubuhi.

¹⁴ Sasa, haidhuru alikufa kiasi gani, na jinsi kifo Chake kilivyokuwa cha kusikitisha, kama hapakuwa na ufufuo, Yeye alikuwa tu ni mtu aliyekufa. Mnaona?

¹⁵ Kumekuwa na watu wengi mashuhuri katika u—ulimwengu wetu, ambao wametoa madai makubwa.

¹⁶ Kwa mfano, Confucius, yule mwanafalsafa mkuu wa Kichina, alikufa yapata miaka elfu mbili mia tatu iliyopita.

¹⁷ Budha, yule nabii-mungu mkuu wa Japani, pia alikufa yapata miaka elfu mbili mia tatu iliyopita; alitoka matamshi makubwa, lakini alikufa. Naye angali kaburini.

¹⁸ Kuna Muhammad, majaliwa ya kuwa kwenye kaburi lake, ambapo, kwa miaka elfu mbili, farasi mweupe amesimama kwenye kaburi lake; wakibadilisha zamu ya walinzi kila baada ya saa nne, wakimtarajia afufuke siku moja, na kuendesha farasi kote ulimwenguni, na kuuteka. Waislamu, ambayo ndiyo dini kubwa zaidi kwa idadi, ulimwenguni. Wamewazidi Wakristo wote, Wakatoliki, wakiwekwa pamoja. Lakini, hata hivyo, Muhammad yuko kaburini.

¹⁹ Na dini hizi zote, tunaposema ya kwamba, “Yesu amefufuka katika wafu,” wanasema, “Lithibitisheni.” Nasi tunasema, “Vema, Yuko moyoni mwetu.” Wanasema waanzilishi wao wako moyoni.

20 Lakini nina furaha sana kwamba Yesu alituachia msingi thabiti, wa mwamba wa ufufuo Wake. Hatupaswi kustaaajabu. Ni Kweli. Jambo la kushangaza ni kwamba, watu wengi hawalioni. Nalo limenishangaza. Na, usiku wa leo, nitajaribu kuliendea kwa Maandiko.

21 Sasa, kama ukiangalia, hawa walikuwa kaburini, asubuhi na mapema. Wakakutana na Watu wawili, ambao walikuwa ni Malaika waliovaa nguo za kumeta-meta, waliowaambia ya kwamba Yeye alikuwa . . . “Kwa nini mnamtafuta aliye—aliye hai katika wafu?” Walikuwa wameenda kaburini wakakuta hayupo. Nao wakauliza swali hili muhimu, “Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Naye akasema, wakati . . . Mambo haya aliwaambia alipokuwa angali Galilaya.”

22 Sasa, labda unaweza kusoma upitie tu juu ya hilo, lakini hebu tulizingatie hilo kwa muda. Alisema, “Aliwaambia mambo haya alipokuwa angali Galilaya.” Kwa nini hawakuyaelewa? Kwa nini hawakuyapata?

23 Na hapa kuna umuhimu mwingine mkubwa kwake, ya kwamba, hawa waliomwambia haya, ama kuwaambia wanafunzi hawa, walikuwa kaburini. Lazima walikuwa pamoja naye pia huko Galilaya, kwa maana walijua kile ambacho Yesu alikuwa amewaambia kabla ya kusulubiwa Kwake. Loo, ni jambo la baraka jinsi gani! Mnaona, hao wanafunzi hawakujua Malaika hao walikuwa pale, lakini hakika walikuwapo, kwa sababu walisema, “Hakuwaambia hayo alipokuwa angali Galilaya?”

24 Na hilo linatimiza yale Maandiko yaliyosema, ya kwamba, “Malaika wa Mungu hufanya kituo kuwazungukia wale wamchao.”

25 Na hilo ni jambo kubwa jinsi gani, kujua kwamba, usiku wa leo, mumu humu kwenye jengo hili, kuna Malaika wa Mungu wamesimama imara. Nao wanajua kila neno tunalonena, na kila tufanyalo.

26 Na hili hapa thibitisho lake la Kimaandiko. Kasema, “Je, hakuwaambi ni mambo haya alipokuwa akaliko Galilaya?” Kasema, “Kumbukeni ya kwamba aliwaambia mambo haya.” Neno hilo, “kumbukeni,” hilo ni neno la ajabu.

27 Na, loo, ni jambo la kuhuzunisha jinsi gani litakalowapata, kwamba baada ya wao kutia muhuri maangamizi yao, na baada ya kusikia mahubiri yao ya mwisho, na kuwa katika jehanamu ya ibilisi, wamepotea, wala hawana nafasi hata kidogo ya kutubu; kukumbuka nafasi walizozikataa.

28 Unaniambia, basi, “Mhubiri, kwani kuna ukumbusho kuzimuni?” Yesu alisema kulikuwako. Alisema yule tajiri aliinua macho yake, kuzimuni, akamwona Ibrahimu, na Lazaro kifuani Mwake. “Naye akasema, ‘Kumbuka, katika maisha yako . . .’” Kuna ukumbusho.

²⁹ Na jinsi ambavyo, waliopotea, lingekuwa ni jambo baya jinsi gani, kujua ya kwamba ile mikutano mikuu waliyokuwa wamehudhuria, na walikuwa wamesikia mahubiri makuu ya watumishi wa Mungu waliotiwa mafuta; isitoshe, bali kuona ishara na maajabu yaliyotiwa mafuta ambayo Mungu alikuwa amefanya miongoni mwa watu; na kisha kukumbuka maonyo haya yote, na hata hivyo wapotee. Mbona, ingewasumbua milele.

³⁰ Baada ya kifo cha Yesu, Biblia inatwambia kwamba, “Alienda akazihubiri nafsi zilizokuwa kifungoni, wasiotubu katika uvumilivu wa siku za Nuhu.” Na kuwakumbusha kwamba Nuhu, na Henoko, na manabii wakuu wa siku zao, walishuhudia ya kwamba yuaja Masihi, nao wakaukataa Ujumbe huo.

³¹ Loo, litakuwa ni jambo baya sana, rafiki yangu uliyepotea, kwako, katika siku hiyo, kukumbuka. Ukifa, hapa, kazi zako zinakufuata. Nazo ama zitakusumbua kote katika Umilele, au kukubariki kote katika Umilele.

³² Lakini, kumbukeni, hapana shaka ni jambo kuu jinsi gani, na furaha, kwa wale waliookoka, na wanaweza kuleta, kukabiliana na ukweli, Malaika hawa walioko humu jengoni usiku wa leo, kukumbuka ile mikutano mikuu na nyakati kuu, na furaha kuu ambazo tumekuwa nazo pamoja. Ni wakati wa jinsi gani uliopo mbele, kwa makundi yote mawili, waliookoka na wasiokoka!

³³ Mungu ni Mungu mwema. Yeye ni mvumilivu sana! Amejaa sana fadhili, na upole, na subira! “Hataki kwamba yeyote aangamie.” Naye amefanya kila kitu kinachoweza kufanywa, kuwazuia watu wasiangamie. Bali wataangamia, kwa vyovyote vile, kwa sababu hawaamini.

³⁴ Sasa, tunachukua somo letu, usiku wa leo, kuwaona watu wawili, baada ya ufufuo. Na wengi walikuwa wamekuja na kunena juu ya kaburi tupu, walikuwa wamesema ya kwamba mwili Wake haukuwepo. Na wanawake wengine walikuwa wamesema kwamba wameona maono ya Malaika, ambao waliwaambia ya kwamba, “Alikuwa amefufuka katika wafu.” Na, hata hivyo, pamoja na ujumbe huu wote, bado watu hawa hawakuamini, nao walivunjika moyo, wakirudi nyumbani.

³⁵ Na kufikiria, kwenye Pasaka ya kwanza, asubuhi ya kwanza ya Pasaka ya kupendeza ya msimu wa kuchipusha, Yesu yu hai miongoni mwa watu, na hawa wakienda zao, wamevunjika moyo, wakitembea njiani, na mioyo yenye huzuni, nao walifadhaika kuhusu kusulubiwa. Ndipo walipokuwa wakitembea, tunaona ya kwamba kuna Mtu fulani aliyetokea kando ya barabara akaanza kutembea pamoja nao. Nao hawakujua Yeye alikuwa ni Nani, kwa sababu Maandiko yanasema ya kwamba macho yao yalikuwa yamefumbwa.

³⁶ Loo, hapa ndipo ninapotaka muone. Hili halikuwa tu jambo lililotukia, bali lilikuwa ni unabii, na kivuli cha jambo fulani ambalo lilikuwa linaenda kutukia.

³⁷ Mnajua, Bwana wetu aliyebarikiwa hakufanya lolote ili tu kujifurahisha. Kila kitu alichofanya kilikuwa na maana. Kila kitu alichofanya kilikuwa cha Milele; hakikufa kamwe; kila msogeo, kila mwendo, kila Neno. Loo, nina furaha sana kwa hilo. Unaweza tu kulishikilia, pamoja na yote yaliyo ndani yako, nalo litadhihirishwa.

³⁸ Basi walipokuwa wakitembea barabarani, Mgeni akajitokeza. Nao, Yeye—Yeye akawaambia, “Mbona mmehezunika hivi?” Wanapaswa kuwa na furaha. Kasema, “Mbona mmehezunika hivi? Na ni mazungumzo gani haya mnayozungumza?” Naye akasema. . .

³⁹ Wakamjibu, “Je, wewe ni mgeni huku Yerusalemu? Hivi hujui mambo ambayo yamekuwa yakiendelea? Tulikuwa na Nabii Jina lake Yesu wa Nazareti. Nasi tulimtumainia, kwamba Yeye angekuwa Mkombozi. Lakini hii ni siku ya tatu; nao watu wetu walimsulubisha.”

⁴⁰ Basi wakaanza kusimulia yaliyotukia, jinsi alivyokuwa amekufa, jinsi walivyokuwa wamemtarajia kuwa Mkombozi mkuu, lakini jinsi yule Nabii wa Mungu Aliye Juu angeweza kusimama pale kwa huruma, na mate usoni Mwake, na kumwacha askari amvike kitambaa kichwani, na kuyapofusha macho Yake, na kumpiga kichwani kwa fimbo, na kusema, “Sasa tabiri, Ewe mtabiri, na utwambie ni nani aliyekupiga. Tutakuamini.” Hiyo ilikuwa ni zaidi ya vile watu wangeweza kuelewa. Walikuwa wakifikiri kwamba Masihi angekuwa kitu tofauti na hicho.

⁴¹ Na ikiwa hiyo siyo picha ya kweli, siku hizi. Watu wanautazamia Ufalme wa Mungu kuwa tofauti na ulivyo kweli. Wanautarajia uje katika fahari. Wanautarajia utokee katika jiji la Vatikani ama kanisa fulani kuu. Lakini kwa sababu Yeye huuleta miongoni mwa kundi la maskini, wasio na elimu, watu wenye mioyo ya unyenyekevu, huyapofusha macho ya wenye hekima na akili.

⁴² Loo, ni dhihaka jinsi gani kwa mwanamke huyo kupitia na kudhihakiwa, akiosha miguu Yake kwa nywele zake, kama yule mwaminio wa kweli alivyokuwa amefanya. Ni dhihaka iliyoje kumwona akining’inia pale msalabani, huku mikono Yake imetundikwa msalabani, na kumsikia kuhani mkuu, kasema, “Sasa, kama Wewe ni Mwana wa Mungu, fanya mwujiza hapa. Vuta tu uifungue mikono Yako, kisha ushuke msalabani, nasi tutakuamini.”

⁴³ Sasa, katika akili ya mwanadamu wa kawaida; mtu wa kimwili, mtu wa kanisa, anayejifanya mwaminio. Kwa sababu, kila kusanyiko lina watu wa aina tatu mbalimbali, hao ni:

mwaminio wa kweli, na anayejifanya mwaminio, na asiyeamini. Kila kusanyiko linao.

⁴⁴ Na kufikiria ya kuwa Mtu huyu, aliyeyafumbua macho ya vipofu, akazibua masikio ya viziwi, na alikuwa amemfufua mtu katika wafu, ambaye alikuwa amekufa siku nne, na angeweza kutoa matamshi kama vile Yeye alivyotoa; halafu angening'inia pale, huku ametemewa mate usoni, na kumwacha kuhani mkuu amwudhi na kumwambia mambo kama hayo, wala hakufungua kinywa Chake na kujibu neno, katika mjadala. Kwa maana alisema, "Sikuzote ninafanya yale yanayompendeza Mungu." Na ilimpendeza Mungu hayo yatendeke.

⁴⁵ Sasa hebu tumtazame kwa dakika chache. Sasa, wanafunzi hawa, wasingeelewa kwa nini hili halina budi kutendeka. Kwa hiyo walipoendelea na safari na kuanza kueleza hiyo hadithi, ndipo Yesu akawakatiza. Mnaona, Yeye aliwatokea walipokuwa wakizungumza juu Yake.

⁴⁶ Na hiyo ndiyo sababu Yeye haonekani kwa watu wengi sana wa kanisa, siku hizi, hawazungumzi habari Zake vya kutosha. Kanisa daima linazungumza juu ya matendo makubwa wanayoendeleza, karamu fulani kubwa ya kijamii, au mandari fulani watakayofanya, ama jambo fulani jipya ambalo watafanya, baadhi ya vyama vya kijamii. Kanisa limelemewa sana na vyama vya kijamii mpaka halina nafasi yoyote kwa ajili ya Kristo.

⁴⁷ Kanisa la kweli daima hujiondolea vyama hivi vyote vya kijamii, na hugeuza kila kitu kuwa mkutano wa maombi, wale wanaomjua na kumpenda.

⁴⁸ Naye Huyu hapa. Walikuwa wakizungumza juu Yake wakati alipotokea.

⁴⁹ Kama tungeacha kuzungumza juu ya majirani zetu, na kuacha kuzungumza juu ya wanafiki kanisani, na kuzungumza zaidi juu ya Yesu, tungekuwa na kuonekana kwingi zaidi kwa Yesu; kuzungumza juu ya makosa ya mhubiri, kuzungumza juu ya makosa ya kitu kingine. Na tuongee tu juu ya Yesu, kungekuwa na mambo mengi zaidi yakitokea.

Sasa, ndipo walipokuwa wakizungumza, Yeye akatokea.

⁵⁰ Na halafu, angalieni, anapotokea, Yeye haanzi kukuunga mkono. "Loo, hiyo ni kweli. *Huyu* anapaswa kuondolewa. Na *hili* linapaswa kuwa na mchungaji mpya. Au, jirani *huyu* alikukosea."

⁵¹ Mnaona, mara alipotokea, alianza kuhubiri Neno. Mtumishi halisi wa Mungu daima huenda kwenye Neno. Alisema, "Enyi msiofahamu, na wenye mioyo mizito kuamini yote waliyosema manabii juu ya Kristo." Mnaona jinsi, hili, alivyolileta? "Hivi ninyi ni wazito sana na wasiofahamu, hata hamkuamini waliyosema manabii?"

52 Vipi kama angetokea, usiku wa leo? Ningependa tu kuuliza hivi. Angefanya nini kwenye Maskani ya Branham, usiku wa leo? Je, ninyi ni wazito sana wa moyo?

53 Angefanya nini Jeffersonville, usiku wa leo, ambapo Injili imehubiriwa kwa miaka ishirini na mitano; ishara na maajabu, miujiza, jambo lisilo na shaka? Mambo ambayo hayajawahi kufanywa tangu Yesu alipoondoka duniani, yanafanywa kila siku. Wagonjwa wanaponywa, ishara na maajabu yanafanyika. Unabii mkuu unatolewa, ambao haushindwi kamwe. Injili inahubiriwa bila kupatana, na bado vyumba vya baa na makelele ya uelevi vimejaa usiku wa leo, Jeffersonville. Loo, tunawezaje kuepuka ghadhabu ya Mungu?

54 Nimesema jambo hili mara nyingi, na bado ninalisema, usiku wa leo. Ikiwa Mungu angetuacha twende bila adhabu, angekuwa Mungu dhalimu. Ingemlazimu kuinua Sodoma na Gomora, na kuwaomba msamaha, kwa kuwazamisha kwa jambo lile lile tunalofanya kila siku, na kuzidi kuwa mbaya. Ingawa, walikuwa ni kundi la wapagani, lakini sisi tunadhaniwa kuwa taifa la Kikristo.

55 Naye alipokuwa akisema nao, na kuanza kuwafafanulia Maandiko, na si kwamba tu alikuwa akiwapigapiga mgongoni na kuwapa fundisho la watoto wadogo, lakini alikuwa akiwakemea, na kusema, “Ninyi hamfahamu, na ni wazito wa moyo. Kwa nini mlitilia shaka aliyosema nabii?” Mnaona alikoenda? Moja kwa moja kwenye Maandiko.

56 Nao wakaanza kutazama na kusikiliza. Akasema, “Je, haikumpasa Kristo kufufuka siku ya tatu, na kuingia katika Utukufu Wake?” Naye alipokuwa akiendelea, siku nzima, akiongea, hata hivyo wao hawakumjua, kwa sababu macho yao yalikuwa yamefumbwa. Yalikuwa yamefumbwa, na wasingeweza kumwona, au, kumwelewa.

57 Sasa, hapa ndipo ninapotaka kufikia, kile ninachotaka muone. Huo ulikuwa ndio ujumbe wa kwanza baada ya ufufuo. Ndipo alipokuwa akitembea nao siku nzima, hawakumtambua. Hata hivyo, alikuwa pamoja nao, lakini Yeye Mwenyewe alikuwa ameyafumba macho yao. Lakini ilipokaribia machweo ya jua, ndipo Yesu akafanya kana kwamba anaendelea mbele.

58 Kama hivyo sivyo hasa Yeye alivyofanya tena katika siku hizi za mwisho, kwenye machweo ya jua. Je, mliona kile alicholipa kanisa wakati huo, siku nzima? Kuhubiri tu Neno. Hakufanya hata ishara moja wala maajabu. Kamwe hakusema lolote ila kuhubiri tu Neno kuhusu ufufuo, juu ya yale nabii aliyosema. Hivyo ndivyo amefanya tangu siku za kuondoka Kwake, mpaka siku hizi za mwisho. Lakini sasa, loo, Jina Lake lihimiwiwe, jua linatua, Naye alifanya kana kwamba asingesimama.

59 Loo, ninaweza kuwazia juu ya Fanny Crosby alipolia, “Usinipite, Ee Mwokozi mpole.”

⁶⁰ Wanafunzi hawa wakasema, “Njoo ukae. Kaa pamoja nasi usiku, kwa maana kumekuchwa.” Naye akafanya kama anataka kuendelea mbele, lakini wakamshawishi. Kwa maneno mengine, walimsihi. Loo, laiti tungelikuwa na watu wengi zaidi wanaosihii!

⁶¹ Dada, ndugu, unajua Biblia ilisema Roho Mtakatifu awatie alama wale tu wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini? Sasa, ninataka kuwaulizeni swali. Tunafanya mihemko mingi juu ya mawazo yetu ya kidini, lakini ni nani aliye mjini, usiku wa leo, katika Jeffersonville, ambaye anauhangaikia sana ulimwengu uliopotea, katika siku hii ya mwisho, ambaye hutumia hata dakika thelathini, usiku, akiomba kwa ajili ya dhambi za mji? Lakini kulingana na Maandiko, Malaika wa Mungu alipaswa kuwatia muhuri wale tu waliougua na kulia kwa ajili ya chukizo.

⁶² Hatujali tena. Tunataka tu kujua kwamba tunaweza kuwa na wakati mzuri. Tunataka kujua kwamba tunaweza kuwa na chama kidogo cha kijamii kanisani mwetu. Tunataka kujua kuwa tunayo ku—kura inayokuja, ukifikia wakati wa kumchagua mchungaji mwingine. Tunataka kanisa letu lionekane bora zaidi kuliko kanisa la mwenzetu mwingine. Hilo ndilo wazo la dunia hii siku hizi. Hakuna anayesihii, “Ee Bwana Mungu, njoo kwangu upesi, la sivyo nitaangamia. Loo, usinipite, Ee Mwokozi. Ulikuwa mweza yote. Wewe uliye kila mahali, njoo ukae moyoni mwangu, Ee Bwana.” Hata ni vigumu kumfanya mwanamume au mwanamke kuinua mkono wao, kumkubali Bwana Yesu kama Mwokozi. Benchi la mtindo wa kale la waombolezaji limeondolewa. Hakuna kulia tena. Hakuna kulia tena madhabahuni.

⁶³ Hebu wazieni tu, wakati Charles G. Finney, mhubiri tu wa Injili, maskini mwanasheria aliyelongoka, maskini jamaa mdogo aliyekauka, alikuwa akijaribu sauti katika jengo moja. Naye akasema, “Tubuni, la sivyo mtaangamia.” Ndipo mtu mmoja aliyeketi kwenye kuba akazimia na kuanguka chini. Alisimama kwenye roshani ya jengo huko New England na kuwahubiria kuzimu waliopotea. Ndipo alipopaza sauti, “Mtaangamia msipotubu,” wanaume walizimia, na wanawake, na kuanguka mitaani.

⁶⁴ Lakini, leo, unaweza kuhubiri toba na kuzimu ya moto na kiberiti, nao watu watayacheka. Kuna nini? Mioyo yetu ni baridi. Hatujali. Tuna mengi kupita kiasi. Tunahitaji machache ya dunia na mengi zaidi ya Mungu. Mioyo yetu ni baridi kupindukia. Tunavutiwa na mhemko fulani. Tunakuwa na hamu, “Laiti—laiti tungaliweza kucheza; laiti tungaliweza kupaza sauti.” Ninaamini hayo. “Laiti tungeweza kunena kwa lugha.” Ninaamini hilo. Ninaamini kila sehemu ya hayo. Lakini kama tuna hayo, wala hatuna roho ile inayougua, inayolia, iliyovunjika, Mungu hawezi kuitumia. Mambo hayo ni mazuri,

lakini hatuna budi kuwa na hayo mengine ya kuambatana nayo. Tumeacha jambo kuu, na kuyaenda ya pili; na kamwe huwezi kuyafanya makubwa mambo madogo. Tunajua hilo.

⁶⁵ Hata katika mikutano yetu wenyewe, mikutano yetu wenyewe imefika mahali ambapo tunatilia maanani sana uponyaji wa Kiungu, badala ya uponyaji wa nafsi. Ndugu, tunachohitaji leo hii ni uamsho wa kuvunjika, mioyo ikiwaka moto kwa ajili ya Mungu. Ninachomaanisha, “kuwaka moto,” ni kuwa chini madhabahuni, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao. Sio kwa dakika tano, na kusimama na kusahau. Lakini huko nje wakijaribu kuwarudisha waliopotea wamrudie Kristo tena; mzigo moyoni mwao.

⁶⁶ Mungu, ondoa anasa zote za dunia, na kashfa zake zote, ucheshi wake wote, na uweke mzigo juu ya moyo wangu kwa ajili ya waliopotea, yangukuwa ndiyo maombi yangu.

⁶⁷ Walimshawishi. “Ee Bwana, hatujui Wewe ni nani, Bwana, lakini tunapenda mahubiri Yako. Karibu, ukae nasi usiku kucha.” Ndipo Yesu akaingia ndani. Alitembea pamoja nao, nao hawakumfahamu. Ndipo mara alipoingia . . . Labda ni kibanda kidogo, lakini hakuna kitu duni sana Kwake.

⁶⁸ Unasema, “Vema, Ndugu Branham, mimi ni mzee.” Sijali wewe ni mzee kiasi gani. “Mimi ni mtoto tu.” Hiyo haijalishi wewe ni mchanga kiasi gani. “Mimi ni maskini sana. Nimevaa ovaroli.” Loo, kama ungalikuwa umezungushiwa gunia la nyasi, isingeleta tofauti kwa Mungu. Mwombe tu. Wewe ni mkuu machoni pa Mungu. Huenda usiwe na faida sana mbele ya watu, lakini wewe ni mkuu mbele za Mungu. Wewe ni mmoja wa raia Wake.

“Karibu ukae nasi.”

⁶⁹ “Loo, nisingeweza kumwomba aingie ndani yangu. Nimekuwa mlevi. Nimekuwa mcheza kamari.” Sijali wewe ni nini. Mwombe, upate kujua. Atakuja kwa mwaliko wako. Hajawahi kumkataa mtu yeyote. Wala kamwe hatamkataa mtu yeyote. Anatamani na kujaribu kuingia mioyoni. Unasema, “Nimekuwa kahaba wa mtaani.” Sijali umekuwa nini. Mungu anajaribu kupata njia ya kuingia moyoni mwako.

Sema tu, “Ingia, Bwana, ukae pamoja nami.”

⁷⁰ Pia angalia, siku nzima, Yeye amekuwa akilileta Neno, lakini bila ishara. Alipowaingiza ndani, na kufunga mlango, na kuketi chini, loo, ndugu, hapo ndipo alipofunua kufufuka Kwake. Hakuna wakati, tangu asubuhi alipokutana nao, mpaka machweo ya jua, alipofanya hivyo. Kamwe hakufanya jambo moja alilofanya maishani, Neno tu. Lakini angalieni, wakati wa jioni, wakati wa jioni, hapo ndipo alipothibitisha kufufuka Kwake.

⁷¹ Hebu niseme hili kwa unyenyekevu. Acha niseme hili kwa sauti iliyovunjika, lakini moyo uliovunjika, pia. Ni wakati wa jioni. Biblia ilisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni. Kutakuwa na siku, ambayo haitakuwa usiku wala mchana,” nabii alisema. Itakuwa ni kusikia tu Neno, bila madhihirisho, siku ya huzuni tu, yenye ukungu. Lakini wakati wa jioni, Nuru itaangaza tena. Itakuwa nuru. Na katika wakati huu wa jioni tunaishi sasa, ambapo Kristo, kupitia wahudumu Wake, amehubiri Injili kwa miaka elfu mbili, lakini hizi ndizo nuru za jioni. Nuru za jioni zilikuwa ndizo madhihirisho ya ufufuo.

⁷² Lini? Hawakujuu alikuwa amefufuka katika wafu. Ingawa walimpenda, walimwamini, lakini hawakujuu alikuwa amefufuka katika wafu. Walikuwa wamebishania jambo hilo. Na sasa, hili hapa katika wakati wa jioni, Yeye atajifunua Mwenyewe, ya kwamba amefufuka katika wafu. Alifanyaje hilo? Sio kwa kuhubiri Neno; tayari alikuwa amefanya hivyo, na bado hawakuamini.

⁷³ Na miaka elfu mbili ya kuhubiri Neno, kanisa bado haliamani. Lakini Nuru ya jioni imekuja, dhihirisho la ufufuo.

⁷⁴ Basi akawaingiza ndani, Naye akafanya mwujiza, ama akafanya jambo kama tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake. Walijua ilikuwa ni Yeye. Macho yao yakafunguka.

⁷⁵ Naye akatoweka, upesi. Angalieni, ulikuwa ni ujumbe mfupi. Haukuwa mrefu sana. Hakukaa nao kwa muda mrefu. Alijidhihirisha tu Mwenyewe, kisha akatoweka machoni pao. Ndipo macho yao yakafumbuliwa nao wakajua ya kwamba huyo alikuwa ni Yeye.

⁷⁶ Nao wakasema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akizungumza nasi njiani?”

⁷⁷ Na, loo, ndugu, dada, ni kiasi gani mioyo yetu imewaka, kote katika miaka. Nimekuwa Mkristo sasa kwa takriban miaka ishirini na saba; la, takriban miaka ishirini na tisa. Nimekuwa mhubiri kwa miaka ishirini na saba. Na wakati wote, ninaposoma Neno Lake, anapozungumza nami, ni ajabu. Moyo wangu unawaka, kulisikia Neno.

⁷⁸ Lakini sasa Nuru za jioni zimekuja. Jua linatua. Ustaarabu umekwisha. Ulimwengu uko mwisho. Sasa ametokea na anafanya jambo fulani katikati yetu, ili kujidhihirisha Mwenyewe kama Kristo aliyefufuka. Macho yetu yanainii, yanaweza kufunguka. Tunaweza kuona kwamba yu hai hata milele. Thibitisho la mlo ni kuula wenyewe. Na hilo ndilo thibitisho la kufufuka. Ikiwa Yesu aliahidi, Biblia iliahidi, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” wala Yeye hathibitishi hilo, basi Maandiko yamekosea. Kote katika miaka tumekuwa na mafundisho haya yote ya Maandiko, lakini hii ndiyo siku ya madhihirisho, kwa madhihirisho ya ufufuo.

⁷⁹ Sasa, walifanya nini? Macho yao yalipofumbuliwa, walisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?” Nao wakakimbia upesi kurudi, kukutana na watu wao wengine. Nao hawakurudi sasa, wakienda zao tu barabarani, na kusema, “Vema, labda inaweza kuwa kitu kingine.” Lakini walikuwa na hakika. Nao wakakimbilia kundi lao wenyewe, wakasema: “Hakika, Bwana amefufuka, kweli! Tunajua kwamba amefufuka.” Hawakwenda kubishania dini yao. Walienda tu kwa sababu macho yao yalikuwa yamefumbuliwa. Walikuwa wamemwona katika kufufuka Kwake.

⁸⁰ Na ni nini kingekuwa kitu cha kupendeza zaidi, usiku huu, rafiki yangu? Ni jambo gani lingekuwa tukufu zaidi, usiku wa leo, katika siku hii ya Pasaka? Ni kumwona Yesu yeye yule aliyefufuka katika wafu, akiingia katikati ya maskini maskani hii nyenyekevu, hapa, ambayo ilitugharimu chini ya dola elfu tatu, miaka ishirini iliyopita. Ingekuwaje, katika mahali hapa padogo, kumwona akija hapa, usiku wa leo, na kufanya mambo aliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, kuthibitisha kufufuka Kwake?

⁸¹ Hajawahi kufanya hivyo mpaka siku hizi za mwisho. Sasa Yeye anafanya hivyo kwa sababu aliahidi angelifanya. Ni wakati wa jioni. Taa zinawaka. Mungu anafungua macho ya watoto Wake. Wao, kwa mioyo myepesi, wanarudi nyuma haraka, “Loo, amefufuka, kweli.”

⁸² Sasa, kuna watu katika jengo hili, usiku wa leo, ambao labda wanatoka Virginia, na kote nchini. Na—na, ama haidhuru unatoka wapi, unaweza kurudi ukiwa na moyo mwepesi, kwenye siku hii ya Pasaka, kama Yesu angekutokea kama alivyowatokea wale.

⁸³ Labda umetembea pamoja Naye kwa muda mrefu. Labda umekuwa Mkristo kwa miaka mingi, lakini bado hujaona nguvu za kufufuka Kwake zikidhihirishwa. Loo, kama atafanya hivyo usiku wa leo, je, utampokea kama Bwana aliyefufuka?

⁸⁴ Liwazie sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi. Ni wangapi wangependa kukumbukwa katika maombi haya? Inua mkono wako kwa Mungu. Mungu akubariki.

⁸⁵ Sasa, Bwana Mungu, watu wamesimama, viungo vyao vinakakamaa. Lakini, loo, wanakupenda Wewe. Wamekuja, Bwana, katika siku hii ya ufufuo. Wamekuja, labda, kutoka kwenye maskini kaburi tupu mahali fulani, ambapo wanahubiri Injili tupu, na kusema, “Vema, siku za miujiza zimepita.” Hivyo ndivyo walivyolikuta hilo kaburi, kwa sababu hakuwemo. Alikuwa amefufuka katika wafu.

⁸⁶ Lakini Kleopa na rafiki yake wanao wengi wanaosafiri pamoja nao, usiku wa leo, wakilijadili, wakienda zao. Lakini, Ee Bwana Yesu, katika nyakati hizi za jioni, ninaomba ya kwamba

utadhihirisha ufufuo Wako kwa kanisa hili dogo, usiku wa leo. Wathibitishie hawa, wanaosimama karibu, kwamba Wewe ni mnyenyekevu. Hiyo ni, ikiwa . . . Haijalishi ni duni namna gani, utakuja mahali popote unapokaribishwa, unapotakiwa.

⁸⁷ Na kuna wengi hapa, Bwana, ambao ni wahitaji. Wengi ni wagonjwa na wengi wanateseka. Wengi wako bila Wewe, bila Kristo, bila Mungu, nao wanataka usaidizi. Ninaomba, Baba, ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe, usiku wa leo, kwenye maskani hii ndogo, mara nyingine tena.

⁸⁸ Ee Bwana Mungu, umekuwa mwema kwa mtumishi Wako. Miaka mingi iliyopita, leo, katika maskini kibanda cha kale cha mbao kilichoonekana duni, wakati mama yangu kijana kule nyuma, mwenye umri wa kama miaka kumi na mitano, alipofungua dirisha, asubuhi na mapema, nami nikatoa kilio changu cha kwanza. Ee Bwana Mungu, nakushukuru kwa ajili ya kila mwaka. Ninaona aibu kwa mambo mengi ambayo nimefanya ambayo ni makosa. Ninaomba unisamehe. Na majuto moja niliyo nayo, Bwana, kwamba sikukutumikia nilipokuwa mvulana mdogo. Nisaidie, Bwana.

⁸⁹ Ee Bwana, ikiwa nimepata neema machoni Pako, utie nguvu mwili huu dhaifu. Zifanye upya nguvu zangu. Fanya upya nguvu za ujana wangu, kama uwafanyavyo tai, na kuinua kichwa changu, Bwana, na kuinamisha moyo wangu chini, ili nipate kutembea, Bwana, bado, na kuudhihirisha upendo Wako kwa watu. Nipe upendo wa kina zaidi, kujiweka wakfu zaidi, kilindi, chenye maisha tele, maisha makamilifu zaidi, ili nipate kukutumikia Wewe.

⁹⁰ Bwana, dhihirisha nguvu Zako usiku wa leo miongoni mwa watu, kwa kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka, ukitoa ushahidi wa kufufuka Kwako. Nasi tutakupa sifa, katika Jina la Bwana Yesu tunaomba. Amina.

⁹¹ Ninaupenda huo, Dada Gertie. Ni wangapi wanaujua, “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi”? Hebu kwa namna fulani tuuvumishe, pamoja sasa, mara moja tu. Napenda . . . Ni wangapi wanazipenda hizo nyimbo za kale? Loo, mnaweza kuzichukua bugi-wugi zenu zote zilizokatakatwa, za Elvis Presley, kwa jina la Ukristo, mnaweza kuzichukua. Nipe zile nyimbo za Injili za mtindo wa kale, zenye kuisisimua moyo, za upendo. Naam, bwana.

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana
Mungu wa majeshi.
Mbingu na nchi zimejaa Wewe,
Mbingu na nchi zinakusifu Wewe,
Ee Bwana uliye Juu Sana.

⁹² Je, hilo haliwafanyii kitu? Abuduni tu sasa, pamoja tu, tunapouimba huo tena sasa. Abuduni tu sasa, kwa Mungu, kwa namna fulani jifungieni, na mwabudu sasa, tunapoimba.

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana
 Mungu wa majeshi.
 Mbingu na nchi zimejaa Wewe,
 Mbingu na nchi zinakusifu Wewe,
 Ee Bwana uliye Juu Sana.

⁹³ Bwana Mungu uliye Juu Sana, Ndiwe uliyeliweka jua katika mzingo wake. Uliweka mwezi, nyota. Uliipima dunia katika kiganja cha mkono Wako, na kuzivumisha nyota. Wewe ni Mungu. Ulimfufua Yesu katika wafu, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, na ukamwonyesha akiwa hai, kutupa hakikisho hilo lililobarikiwa, kwamba tungojee sasa Kuja Kwake Yeye atakayeketi juu ya kiti cha enzi cha Daudi na atatawala dunia kwa amani na uadilifu. Hatutajifunza vita tena. Hakutakuwa na njaa wala huzuni tena. Hakutakuwa na huzuni tena, hakuna mauti tena. Mambo ya kwanza yatapita. Na, Ee Mungu, kumekaribia sana!

⁹⁴ Itie nguvu mioyo ya watoto Wako. Utupe, usiku wa leo, shauku zetu. Si kwa ajili yetu wenyewe, Bwana, bali ili tuwe na ushuhuda mpya mioyoni mwetu wa kufufuka Kwake. Ninaunyenyekeza moyo wangu na kukuomba Wewe unisaidie. Nao wasikilizaji wanainyenyekeza moyo yao na kukuomba Wewe uwasaidie, ili kwa pamoja tupate kumwona Bwana aliyefufuka.

⁹⁵ Njoo katikati yetu, Bwana. Litakase kanisa hili. Naomba rehema za Mungu. Bwana, usituhukumu. Hatuombi hukumu. Tunaomba rehema. Utupe rehema, Ee Mungu wa Milele, na udhihirishe upendo na Uwepo Wako pamoja nasi. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁹⁶ Loo, ninajisikia tu kuabudu zaidi. Moyo wangu umejaa tu! Ni hakikisho la jinsi gani! Yesu amefufuka katika wafu.

⁹⁷ Sio hadithi kama ya Baba Krismasi. Ikiwa ninasema jambo baya mbele ya watoto Wako, unisamehe; simaanishi kufanya hivyo. Lakini ninaamini katika kuwaambia watoto ukweli. Mnaona?

⁹⁸ Nataka kujua Ukweli. Waliniambia habari za Yesu. Ikiwa Yeye hajafufuka katika wafu, basi ni hadithi ya uwongo. Kama Yeye si yule yule jana, leo, na hata milele, basi ni hadithi ya uwongo. Basi, anaweza kuwa amekufa, endapo hatajithibitisha Mwenyewe kuwa Mungu aliyefufuka.

⁹⁹ Lakini nina furaha sana kujua ya kwamba amefufuka katika wafu, na anaishi sasa. Yuko hapa. Na mchanga huu mtakatifu, kama nilivyouzungumzia asubuhi ya leo, hakuna mtu awezaye kuuondoa huo moyoni mwako. Mungu na ayafumbue macho yako, usiku wa leo, ewe msafiri, na kukujulisha kwamba Mwanawe amefufuka katika wafu, na yuko hapa kujidhihirisha Mwenyewe.

¹⁰⁰ Sasa, nilimwuliza Billy ni wangapi walipaswa kuombewa. Hakujua. Ni wangapi hapa wanaotaka maombi, miili iliyo migonjwa, inueni mikono yenu, kote katika jengo. Kila mahali jengoni, ambao wanataka. Wangukuwa wengi kupita kiasi, mnaona, ni zaidi. . . Ni theluthi mbili ya kusanyiko. Isingewezekana kujaribu kuupitisha mstari wa maombi. Tusingeweza kufanya hivyo. Nilimwambia asambaze kadi. Nasi tutajaribu kuwapanga na kuwapitisha, wengi kadiri tuwezao. Na nadhani. . . Ulisambaza mia moja? Vema. Naam, amesambaza kadi mia moja, wala hili jengo halikai zaidi ya mia mbili na hamsini, nadhani, ama kitu kama hicho. Kwa hiyo, pengine, wengi hapa. . .

¹⁰¹ Ni wangapi ambao hawana kadi ya maombi, nawe unataka Mungu akuponye? Inueni mikono yenu, kila mahali jengoni, wasio na kadi ya maombi. Karibu nusu yao. Vema. Sasa kuna njia moja tu halali ambayo tunaweza kufanya.

¹⁰² Kuna kitu akilini mwangu. Kuna kitu moyoni mwangu. Siwezi kusema mpaka nijue ninachozungumzia. Ninaomba. Ninamshikilia Mungu. Ninarudi upande wa nyuma ya jangwa. Si—si—sina budi kukutana na Mungu tena. Kuna kitu fulani tu. Sina budi kwenda kwenye mchanga huo tena, nilikokuwa miaka michache iliyopita. Ninataka kuzungumza Naye. Ni—nilimwona katika ono, mara mbili. Natumaini ninaweza kumwona tena kabla sijaondoka. Kuna kitu nilichopata katika Maandiko. Si—si—sijui. Kimekuwa moyoni mwangu. Na kila wakati ninapozungumza juu yake, jambo fulani hutokea. Nami ni ninii tu. . . niko kwenye. . . Ni—niko mahali, sijui la kufanya. Ninaamini huduma hii niliyo nayo sasa inafifia, kwamba jambo kubwa zaidi litachukua mahali pake. Juma hili lijalo au mawili, ninaenda kwenye mchanga mtakatifu, nikiweza, upande wa nyuma ya jangwa, ili kuona kama ninaweza kuwasiliana na Bwana wangu. Siwezi kupumzika, siwezi kuwa na amani, mpaka nimpate Yeye, mpaka nipate kujua hii yote inahusu nini. Siwezi kuelewa. Hajawahi kunikatalia bado; siamini atanikatalia wakati huu. Najisifu. Ninamuomba anisaidie.

¹⁰³ Si kwamba si—si—sitaki. Jamani, ningeweza kurudi hapa na kuhubiri, na kuendelea sasa. Nakisia nina marafiki wa kutosha wa kusaidia kunitunza. Hivyo sivyo. Hilo silo wazo. Huduma hii niliyo nayo, ningeweza kuendelea, kama Mungu angekuwa pamoja nami. Ningeweza kuendelea.

¹⁰⁴ Lakini moyo wangu haujaridhika. Kuna kilindi kinachoita Kilindi. Kuna kitu kinachosogea. Inaonekana naweza kuweka mikono yangu juu yake, lakini, “Iko wapi, Bwana?” Sio kwa ajili yangu. Ni kwa ajili ya watu Wake. Ni kwa ajili ya watoto wa Mungu. Ninakuwa tu kafara.

¹⁰⁵ Mimi ni mzee. Siku zangu zi—zimekwisha. Siku za ujana wangu zimekwisha. Mtu mwenye umri wa miaka arobaini na tisa

si mtoto tena. Tunajua hilo. Mwaka mmoja zaidi na nitakuwa na hamsini. Mimi si mvulana. Nina watoto wa kulea. Hiyo ni kweli.

¹⁰⁶ Lakini, ndugu, ninayo kazi ya Mungu ya kufanya, juu ya kila kitu. Lazima nijue shauku hii ndani yangu inahusu nini. Sina budi kwenda mpaka niipate. Sina budi kumpata Yeye, mahali fulani. Sina budi kujua.

¹⁰⁷ Nadhani kuna wengine wanaoketi hapa, kutoka yapata miaka kumi ama kumi na miwili iliyopita, kutoka kwenye maskani hii, wakati nilipotoa tamshi hilo hapa wakati mmoja. Ni wangapi hapa ndani wanaokumbuka hilo? Angalieni tu mikono ya zamani iliyosalia. “Kitu fulani hapa ndani,” nilisema, “kuna kitu, karibu naweza kukigusa. Kimekaribia.” Sikujua, baada ya Malaika kunena hapa chini mtoni, mbele yenu nyote, na kusema, “Kama vile Yohana alivyotumwa kama mtangulizi wa Kuja mara ya kwanza, utapeleka Ujumbe kote ulimwenguni.” Imetokea. Kila taifa lina ibada za uponyaji zinazoendelea sasa, kote ulimwenguni, hata zikaingia Urusi. Naam, bwana. Kila mahali, ibada za uponyaji zikiendelea, ambapo zilikuwa zimekufa.

¹⁰⁸ Sasa kuna jambo kubwa zaidi, linalojonga. Kuna... Ninangojea kusikia uvumi wa majani ya miforsadi. Ninaendelea mbele. Niombeeni.

¹⁰⁹ Sasa, kwa kuwa niko katika huduma hii, dhihirisho la kufufuka kwa Yesu Kristo. Ikiwa yu hai, Yeye hutimiza kila ahadi. Ni nani aliyemweka hai kwa miaka hii elfu mbili? Ni nani aliyeifanya hiyo Nuru ya Milele iendelee kuwaka? Sasa ni nyakati za jioni. Madhihirisho Yake ya kitu alichofanya, kama alivyofanya kabla ya kusulubiwa, Alijidhihirisha Mwenyewe kwa wanafunzi. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Walitambua, upesi, huyo alikuwa ni Yeye. Sasa Yeye atafanya vivyo hivyo.

¹¹⁰ Ni wangapi wamehudhuria mikutano yangu mingine? Hebu tuone mikono yenu, kote jengoni. Nadhani ni asilimia mia moja, kwa hivyo sitalazimika kuipitia. Mnajua cha kutarajia.

¹¹¹ Ni wangapi wanaotamani na kungojea kumwona Yeye tena, usiku wa leo, akitembea jukwaani, “Je, Wewe ni Yesu aliyefufuka?” Mungu awabariki. Sasa ili tu kuonyesha kwamba Yeye yu hai.

¹¹² Ilikuwa ni nini? [Mtu anasema, “X.”—Mh.] Ati X? Sawa. Hebu tuninii tu... Hatuwezi kuwaita wengi mno, kwa wakati mmoja. Tunaweza kusimamisha, labda, wanne ama watano kwa wakati mmoja, ama chochote kile. Vema.

¹¹³ Hebu tuanze na kadi za maombi sasa, na tuanze kuwasimamisha. Hebu tuchukue namba moja. Nani anayo? Angalia kadi yako. Namba moja. Moja? [Mtu fulani anasema, “Papa hapa, Ndugu Bill.”—Mh.] Loo, samahani. Sawa, mama. Moja. Namba mbili. Namba tatu. Je, unaweza kusimama, yeyote aliye na namba tatu? Namba nne. Namba tano. Namba sita.

Sioni namba sita. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Namba sita. Vema. Namba saba. Namba saba, tafadhali. Papa hapa. Kwa hiyo, nane, namba nane. Namba tisa. Vema, bwana. Namba kumi. Nyuma. . . Hebu tuone ni wangapi tunaninii. . . [“Ile pale kumi.”] Vema. Hebu tuanze papo hapo, ndipo tunaweza kuona, labda tunaweza kupata wengine wachache.

¹¹⁴ Ni wangapi humu jengoni wasionijua mimi? Sikujui, nawe unataka Mungu akuponye, inua mkono wako. Wote wanaojua kuwa siwajui. Vema. Iweni tu na kicho.

¹¹⁵ Sasa, Bwana wetu Yesu, alipotembea duniani. . . Wakati wakiwapanga watu. Bwana wetu Yesu, alipotembea duniani, hakudai kamwe kuwa mponyaji. Ni wangapi wanaojua hilo? Alisema, “Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu.” Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye alisema, “Siwezi kufanya neno kwa nafsi Yangu; bali lile nimwonalo Baba akifanya, ndilo alitendalo Mwana”?

¹¹⁶ Sasa, na alipompata mtu katika ninii—ninii. . . mtu. Naye akajitangaza Mwenyewe mbele ya jamii ya Wayahudi. Alifanya mwujiza, kwa kumwambia huyo mtu mahali alipokuwa na kile alichokuwa akifanya. Nao wakamwamini.

¹¹⁷ Ndipo alipojitangaza Mwenyewe kwa jamii ya Wasamaria, akamwambia huyo mwanamke siri yake, naye akamwamini, na jamii yote. Je, hiyo ni kweli?

¹¹⁸ Lakini kumbukeni, Yeye kamwe hakufanya hivyo kwa Mmataifa, kamwe hakufanya mbele ya Mmataifa. Kwa sababu. . . Ni wangapi wanaojua ya kwamba hiki kimekuwa ni kipindi cha wakati wa Mataifa? Lakini Nuru za jioni zimekuja sasa. Ni Nuru ya aina gani inayoangaza? Ni Nuru ya aina gani inayoangaza Mwana anapotua? Mwana yule yule aliyeangaza Mashariki wakati lilipochomoza. Mnaamini hilo? Je, huyo ndiye Mwana yule yule aliyepita duniani kote? Mwana yule yule aliyechomoza na kuonyesha Nuru hapa nyuma. Na kulikuwa na giza mchana, siku yenye ukungu tu; halafu, kabla tu Mwana hajatua, akaangaza tena. Ingebidi iwe ni Nuru ile ile iliyoangaza kule nyuma. Ingemmulikia Msamaria na Myahudi, kule nyuma, wala si kwa Mmataifa; basi hana budi kuangazia Nuru ile ile juu ya Mataifa, kusudi awe yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli? Sasa, wewe amini.

Sasa Dada Gertie, kwa utulivu sana, kwa muda kidogo tu.

¹¹⁹ Sasa, katika mstari huu wa maombi, kuna wengi wenu, nadhani, sijui. Ni wangapi wenu hapo ndani, ambao sijui mna shida gani, ama lolote kuwahu? Mnajua hivyo. Inueni mikono yenu, ninyi mlio katika mstari wa maombi, mnaojua ya kwamba sijui lolote kuwahu.

¹²⁰ Ni wangapi katika kusanyiko wanaojua kuwa sijui lolote kuwahu. Sijali kama uko karibu hapa, sasa, sijui lolote kukuhusu. Vema. Vema. Amini tu.

121 Sasa, Bwana wetu alikuwa akienda wakati mmoja ku—kumfufua msichana mdogo, aliyekufa, ndipo mwa—mwanamke fulani akagusa vazi Lake. Naye akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?” Na kila mtu akanyamaza. Walikana kumgusa. Lakini akaangalia pande zote. . .

122 Na baadhi yao wakamkemea, Petro, na kusema, “Bwana, unawezaje kusema ni nani ‘aliyekugusa’ Wewe, huku umati wote unakugusa?”

123 Akasema, “Lakini na—na. . .Nguvu zimenitoka,” yaani, “uweza.”

124 Naye akatazama pande zote mpaka akampata yule ambaye. . .Alijua huyo mwanamke alikuwa ni yupi? Ilikuwa ni imani yake mwenyewe; kwa sababu, Yeye alisema hivyo. “Imani yako imekuokoa. Kutokwa kwako na damu, ambako umekuwa nako, kumekwisha. Imani yako imekuponya.”

125 Huyo ni Yesu Kristo leo, aliyekuwa jana. Kama anaweza kufanya jambo lile lile leo, basi anajithibitisha Mwenyewe vivyo hivyo.

126 Inaonekana kama ninapaswa kumjua mwanamke huyu hapa. Je, wewe ndiye mtu wa kwanza? Je, wewe ni. . .huenda ikawa nakufahamu. Sikujui wewe. Uso wako unaonekana unaojulikana. Sijui. Lakini, chochote kile, simama uje hapa kwa dakika moja. Ninataka kusema, ikiwa ninakujua. . . Labda sikujui. Sijui jina lako. Lakini inaonekana kama nimekuona, na labda nimekuona. Lakini sijui kilichokuleta hapa. Sina fununu kwa nini uko hapa. Wala sijui kama ninakujua. Lakini inaninii tu. . .Inaonekana kama ninakujua, uso wako. Je, ningekujua? Wewe—wewe, nisingekujua. Vema, basi wewe ni mgeni. Uso wake ulionekana unaofahamika kwangu. Sikujua tu. Nilitaka kuwa na hakika.

127 Sasa kila mtu anafahamu, kama wewe ni wa kiroho, hata kidogo, kwamba jambo fulani linaendelea sasa hivi. Loo, hivi—hivi hamwezi tu. . .Hampaswi kuihisi, bali mnaihisi. Ninajua ya kwamba Malaika huyo wa Mungu yuko papa hapa kwenye dawati hili. Mnaiona ile picha pale, ile Nuru? Hiyo Nuru iko hapa sasa.

Unasema, “Mimi siioni.”

128 Wala hawakuwaona wale Malaika waliowaambia, “Aliwaambia hayo akaliko Galilaya.” Walikuwepo.

129 Naye Yuko hapa. Yeye ni Kristo, Yule aliyefufuka. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Kristo yuko katika umbo la Nuru, siku hizi? Hakika. Biblia ilisema ndivyo alivyo.

130 Sasa iweni na kicho sana sasa. Msisogeoesgee. Popote mlipo, ombeni tu.

131 Sasa kama hatufahamiani. . .Na Bwana Mungu, ikiwa Yeye. . .Ikiwa wewe ni mgonjwa, na kama ningeweza

kukuponya, ni—ningefanya hivyo; lakini siwezi. Siwezi kukuponya, kwa sababu tayari limefanywa. Yesu alifanya hivyo alipokufa pale Kalvari, akafufuka. Alithibitisha hilo. Na sasa, kama Yeye atanifunulia kile kilichokuleta hapa.

¹³² Sasa, kama angalikuwa amesimama hapa, amevaa suti hii, angeweza kujua wewe ulikuwa nani. Angejua, kama Mungu alimfunulia. Yeye alisema, “Sifanyi lolote mpaka Baba anionyeshe la kufanya.” Na kama angekuwa hapa, na angekufunulia, labda kuwa wewe ni nani, unatoka wapi, jina lako ni nani, ulichofanya kabla hujahudhuria ibada, ama ulicho nacho moyoni mwako, ama kitu kama hicho. Lakini, kwa uponyaji, ni kazi iliyokamilika. Imekamilika tayari. Sasa, kama atafanya jambo lile lile, je, utaamini ya kwamba utapata kile unachoomba?

¹³³ Kusanyiko litamwinulia Mungu mkono wenu, kwamba mtaamini, pia, iwapo atamfunulia mwanamke huyu? Hebu awe mwamuzi.

¹³⁴ Sasa kama mtu yeyote anataka kuja kupachukua mahali hapa, umekaribishwa.

¹³⁵ Sasa hapa ndipo nitapatikana kuwa mwongo, na Neno la Mungu si kweli, ama ninasema Kweli na Neno Lake ni la kweli. Sawa. Haya basi. Haiwezekani kabisa—haiwezekani kabisa kulikwepa hili. Hii inalionyesha. Hii inalifanya.

¹³⁶ Sasa ikiwa huyu mwanamke ni mgonjwa, nami nimwekee mikono yangu, niseme, “Utapata afya, dada,” ana neno langu tu kwa jambo hilo. Lakini kama Roho Mtakatifu akifunua jambo fulani ambalo limekuwa maishani mwake, huko nyuma, anajua kama hiyo ni kweli au la, jambo ambalo limekuwepo. Ikiwa anajua yaliyokuwepo, bila shaka atajua yatakayokuwako. Hivi hamwamini hilo?

¹³⁷ Sasa na akujalie, dada yangu. Halafu kusanyiko lote limesema wangeamini.

¹³⁸ Na mimi na wewe, hatufahamiani, pamoja, na tunakutana tu hapa kwa wakati huu; wewe ukisimama hapo, kuna kasoro. Sijui ni nini. Sijui. Kwa maana sikujui wewe, basi ningejuaje kile—kile ulicho, shida uliyo nayo? Lakini Mungu anajua shida yako.

Sasa iweni tu na kicho.

¹³⁹ Sasa, huyu mama hayuko hapa kwa ajili yake mwenyewe, kwanza kabisa. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine; huyo ni mtoto. Naye ana shida ya . . . Ana fadhaa sana. Ni mjukuu wako, naamini. Na kuna kitu cha kigeni. Ninamwona mtoto huyo katika mji ambao sio mji huu. Inaonekana kama New Albany. Hiyo ni kweli. Na ana ugonjwa wa fadhaa. Kuna kasoro kwenye ini lake, ndivyo wasemavyo. Anatapika sana. Hiyo ni kweli. Umefadhaika juu yake, nawe umesimama kwa ajili ya huyo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

140 Wewe kuwa mwamuzi. Je, mambo hayo ni ya kweli? [Dada huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Sijui nimekwambia nini. Kanda inajua. Inasema. Itaniambia. Sasa, ilikuwa kwa ajili ya mtu mwingine, kwa njia fulani. Weka lesa hiyo juu ya mtu mwingine, uliyokuwa nayo mkononi mwako wakati upako huo ulipokuwa juu yako, wala usiwe na shaka, nawe utapata kile unachoomba. Kama anajua kilichokuwako, anajua kitakachokuwako. Usiwe na shaka. Nenda, ukiamini.

141 U hali gani, bwana? [Ndugu huyo anasema, “Bwana asifiwe.”—Mh.] Nadhani hatufahamiani. [“Kweli kabisa.”] Hatufahamiani.

142 Amesema hajawahi kuniona hapo awali, maishani, hadi asubuhi ya leo. Sasa, kila mtu awe na kicho sana sasa. Upako tayari unaingia sasa, mnaona. Laiti ningeweza kueleza hili.

143 Lakini Mungu anakujua, bwana. Na kama Bwana Mungu atanifunulia shida yako ni nini, je, utamkubali Yeye kama mponyaji wako, au Mwokozi, chochote unachomhitajia? Utaweza? [Ndugu huyo anasema, “Hakika nitamkubali.”—Mh.] Sasa ono litakapoingia, wewe lisikilize tu.

144 Unajaribu kuvuka sakafu. Na ni kitu fulani gotini mwako. Ni yabisi kavu gotini mwako. Una shida, pia, na macho yako. Yanazidi kudhoofika. Pia una shida na sikio lako. Na una shida kwenye tumbo lako. Hiyo ni kweli. Hutoki kwenye mji huu. Unatoka Somerset, Kentucky. Jina lako ni Bw. Hudson. Sasa rudi, amini kwa moyo wako wote, nawe utaponywa. Amini kwa moyo wako wote.

145 Mnaamini kwa moyo wenu wote, kila mtu? Mwaminini Mungu. Msiwe na shaka, lakini aminini tu.

146 Bwana Mungu anakujua, dada. Je, unaamini angeweza kunifunulia kile kilichokuleta hapa? [Dada huyo anasema, “Ninaamini. Najua hivyo.”] Ikiwa atafanya hivyo, je, utakubali? [“Ndiyo.”]

147 Jamaa huyu mkubwa anayeketi hapa, naam, ninaamini hatufahamiani, bwana. [Ndugu huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Lakini dakika chache tu zilizopita, nilipokuwa nikizungumza na mtu yule, jambo fulani lilikupata. Ulisema moyoni mwako, “Naamini hilo.” Hiyo ni kweli, siyvo? [“Amina.”] Ikiwa Bwana Mungu atanifunulia kile unachotaka uponywe, je, utakubali? [“Naam.”] Una namna fulani ya kikohozi ambacho kinakusumbua. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Vema. Ikiwa utaamini, hutakuwa nacho tena. Kitakuacha. Amini.

148 Aligusa nini? Alifanya nini? Alimgusa Kuhani Mkuu, sio mimi. Hiyo inaweza...Sijawahi kumwona mtu huyo. Sijui chochote kumhusu.

149 Je, unaamini kuwa ni Yesu aliyefufuka? Je, hili si ni jambo lile lile alilofanya baada ya kufufuka Kwake, kuthibitisha ya

kwamba Yeye alikuwa ni Yule yule? Wengine wanasema, “Ni roho ya aina gani hiyo?” Roho daima itajishuhudia yenyewe. Ninii . . . Sisi ni matawi; Yeye ni Mzabibu. Tawi la boga litazaa maboga; tawi la mzabibu litazaa zabibu; mtofaa utazaa matofaa. Maisha ya Kikristo yatamzaa Kristo. Si jambo la ajabu.

¹⁵⁰ Macho yako yanaharibika, nawe unataka maombi kwa ajili ya jicho lako. Hiyo ni kweli, sivyo? Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Unaona, sikujui, lakini Mungu anakujua. Lakini maisha yako, huwezi kuyaficha.

¹⁵¹ Hapa, naona kitu kingine, hospitali. Sasa hebu kidogo. Sio uchunguzi wa jicho. Sio. Ni upasuaji. Sio wewe. Ni rafiki yako, ambaye amefanyiwa upasuaji. Na hicho ni kitu fulani, upasuaji wa henia, nawe unauogopa, kwa sababu unajua ilikuwa ni kitu tofauti na henia. Hiyo ni kweli. Hiyo ilikuwa huko Corydon, Indiana. Hiyo ni kweli. Unaamini sasa kwa moyo wako wote? [Dada mmoja anasema, “Hakika ninaamini.”—Mh.] Nenda, ukapokee ulichoomba, katika Jina la Bwana Yesu.

¹⁵² Najua sura yako. Ikiwa sijako- . . . Bila shaka, huu ni upako, unaona. Lakini, ninavyokumbuka vizuri sana, wewe si ni mhubiri? Unaona, nilitaka tu kujua, ili kwamba ku—kusanyiko lione sio kitu . . . Ni kitu fulani tu, ninapomjua mtu yeyote, na—nawajua. Lakini sijui uko hapa kwa sababu gani. Sina fununu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sijui uko hapa kwa sababu gani. Lakini najua wewe ni mhubiri kutoka mbali huko karibu na Blackiston Mill, ama mahali fulani huko nje. Kwa sababu, ulikuja nyumbani kwangu wakati mmoja, naamini, kumwomba mtoto mchanga ama chochote kile. Hivi . . . Naam. Najua ilikuwa kitu fulani kuhusu mtoto mchanga. Naam.

¹⁵³ Lakini unaugua ugonjwa fulani katika matumbo yako. Acha nikwambie, ndipo utajua kama mimi ni mtumishi wa Mungu au la. Una mtu fulani moyoni mwako, wa kumwomba, na huyo ni msichana kiwete. Yeye hayupo hapa. Yuko ng’ambo ya mto. Yuko Kentucky. Sasa amini kwa moyo wako wote, unaweza kupata kile unachoomba. Amina.

¹⁵⁴ Unaamini? Ikiwa unaweza kuamini, unaweza kupokea. Usiwe na shaka. Vipi kuhusu huko nyuma kwenye kusanyiko? Je, mnaamini?

¹⁵⁵ Huko nyuma kabisa, mwanamke mweusi anayeketi tu upande wa kushoto, ana ugonjwa wa kike, anayeketi ndani, upande wa kushoto. Kama unaamini kwa moyo wako wote, mama, unaweza kupokea uponyaji wako. Je, unaamini? Hiyo ni kweli. Huyo mwanamke mweusi anayeketi karibu na nguzo, kando ya mwanamume. Ameinua mkono wake sasa. Una ugonjwa wa kike. Vema. Bwana Mungu amekuponya, dada. Imani yako ilikuponya.

¹⁵⁶ Hivi hamwezi kuiona Nuru hiyo inayoning’inia juu ya mwanamke huyo hapo? Angalieni hapo.

157 Loo, ni ajabu jinsi gani! Bwana Mungu hashindwi kamwe. Iweni na kicho. Loo, nina furaha sana Yeye yu hai. Anaishi ndani ya mioyo yetu.

158 “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

159 Nadhani sisi hatufahamiani. Sikujui wewe. Sijawahi kukuona. Lakini Mungu anakujua. Ikiwa nimewahi kukuona, sikujua. Lakini ikiwa Bwana atanifunulia kilichokufanya usimame hapa, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, uamini kwamba amefufuka katika wafu? Ikiwa hatufahamiani, itabidi kuwe na aina fulani ya uwezo kunifunulia hilo, lililokuleta hapa. Uko hapa kwa sababu ya mshipa uliovimba ambao unaombea. Hiyo ni kweli.

160 Sasa mwombe mtu mwingine, uone kama mimi ni mtumishi wa Mungu. Mwombe tu mtu mwingine, na uone kama Yeye anaweza kulifunua.

Unaamini?

161 Vema, ana wasiwasi, pia ana shida ya figo. Naye anaishi Corydon. Hiyo ni kweli, sivyo? Basi, unaamini? Sasa nenda ukapokee kama tu ulivyoomba.

162 Nakuuliza. Ninaisahi imani yako kuliadini. Popote jengoni, haidhuru uko wapi, amini tu.

163 Kote huko nyuma, yule kijana mwanamume anayesimama kule nyuma, akimwombea rafiki yake huko Fort Wayne, ambaye ni kipofu. Unaamini Mungu atamponya? [Ndugu huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Vema, basi unaweza kuupokea.

164 Baadhi yenu wengine huko nyuma, aminini. Huko nyuma, nyuma kabisa, aminini. Mpe changamoto, mpe changamoto. Mungu akurehemu.

165 Huyu mama mweusi anayeketi papo hapo chini yako hapo, akiwa na uvimbe. Unaamini Bwana atakuponya, mama; papo hapo kwenye kiti cha nyuma, kiti cha nyuma kabisa huko, kofia ndogo ya mviringo, akiinua mkono wake juu? Unaamini Mungu atakuponya uvimbe huo? Kama unaamini, inua mkono wako na kumpungia Yeye. Vema. Kisha nenda nyumbani ukapone.

Oh, Yeye ni wa ajabu!

166 Huyu hapa mama ameketi papa hapa mbele yake hapa, ameketi upande wa ndani, nyuma kidogo tu. Anamwombea mtu mwingine. Huyu hapo Malaika wa Bwana amesimama karibu naye. Na huyo rafiki yake, anayeomba... anayemwombea, haishi hapa. Ni katika mji mdogo ambapo kuna miti mingi ya misonobari kuuzunguka. Huko ni Henryville, Indiana. Naye anamuombea shemeji yake ambaye ana shida ya moyo. Je, unaweza kuamini? Kama unaweza kuliadini, ukiketi hapo nyuma, mwamini Mungu na uupokee. Vema.

167 Sawa, mama. Hatufahamiani. Sikujui, lakini Mungu anakujua. Kama unaamini, inua mkono wako, mama. Yule mama aliyevaa miwani pale. Vema, ndivyo hivyo.

168 Waonaje? “Bwana Mungu wetu, Yeye ni Mungu.” Hajafa. Yeye hajafa, bali Yu hai. Sio tu kwamba Yu hai, bali Yupo hapa.

Je, huyu ni . . . [Mtu fulani anasema, “Naam.”—Mh.]

169 Je, sisi hatufahamiani, nadhani? Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana, nadhani. Lakini Mungu anatujua sote wawili. Unaogopa nini sana? Pia acha kuwazia juu ya harufu hizo na manukato, na kadhalika. Achana nazo. Mwamini Mungu tu. Unayo tu akilini mwako. Rudi nyumbani na uwe mzima, kama unaamini.

170 Umekuwa na shida. Nakuona ukiingia na kutoka hospitalini; upasuaji mara moja, mbili, tatu. Na hiyo imekuwa kwa utumbo mpana. Ni kitu kama vivimbe, kwenye utumbo mpana. Nawe sio wa mji huu. Wewe ni Mkentaki. Na wewe unatoka katika mji ambao nimekuwako, Campbellsville. Bibi Vaughn, wewe rudi, na ukiliamini. Unaweza kupata kile unachoomba.

171 Unaamini kwa moyo wako wote?

172 Unataka kwenda kula chakula chako cha jioni na kupata ushindi juu ya shida ya tumbo? Sawa, endelea. Wewe mwamini Mungu.

173 Unataka kuondokana na ugonjwa huo wa yabisi kavu na kuponywa? Nenda zako tu, amini.

174 Je, unaamini Mungu ataponya ugonjwa huo wa moyo? [Ndugu mmoja anasema, “Hakika.”—Mh.] Nenda zako. Amini.

175 Mtu huyu anayeketi papa hapa mwishoni, mwenye shati jeupe. La, huyu ni Ndugu Funk. Ni nyuma yake tu. Unataka ubatizo wa Roho Mtakatifu, sivyo? Sawa. Kama utaamini, unaweza kumpokea. Amina.

176 Unaonaje, maskini mama uliyeketi hapa mwenye ugonjwa wa yabisi kavu, ukinitazama usoni? Wewe, kutoka Middletown, Ohio. Unataka kuamini? Hiyo ni imani nzuri, kwa mtu ambaye hata si Mkristo. Hukiri kuwa Mkristo. Hiyo ni kweli. Unamkubali sasa kama Mwokozi wako? Unamwamini na utamkubali kama Mwokozi wako, Bwana aliyefufuka? Sikujui. Sijawahi kukuona. Hiyo ni kweli. Lakini kama utamkubali kama Bwana wako aliyefufuka, sasa hivi moyoni mwako, dhambi zako zimesamehewa, na Mungu atakuponya. Mwinulie mkono wako na kumwamini. Vema. Nenda zako, na ushangilie.

Ninaisahi imani yenu. Ninawasahi kuamini.

177 Hatufahamiani, lakini Mungu anakujua. [Ndugu huyo anasema, “Ninakujua, lakini wewe hunijui.”—Mh.] Unanijua, lakini sikujui. Je, ndivyo hivyo? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia kile kilichokuleta hapa? [“Amina.”]

178 Vema, ni wangapi wataamini?

179 Loo, mnawezaje kukosa kuamini? Hivi Mungu hawezi. . . Je, Mungu amewahi kuyafungua macho yenu? Wengi wenu watu hapa mnanijua. Nililelewa hapa pamoja nanyi. Ningewezaje. . . Rudini nyuma katika maisha yangu, muone kama jambo lolote liliwahi kusemwa ila lililotimia kikamilifu kuwa ni Kweli. Lichunguzeni muone kama si kweli.

180 Naam, ninawaambia nini? Yesu Kristo amefufuka katika wafu. Yu hai. Yuko hapa. Hii ni Pasaka. Na imekuwa Pasaka kwa miaka elfu mbili. Lakini Nuru za jioni zinawaka sasa. Iliwaka Mashariki wakati huo, inawaka kutoka Magharibi sasa.

181 Bwana, hii inaweza kuendelea kwa saa kadhaa. Mtu huyo akisema kwamba simjui. . . Ameniona pengine mkutanoni sehemu fulani au mahali fulani. Sijui. Mungu anajua. Sijui. Sijui mahali nimepata kumwona. Sijui kama niliwahi kumwona. Lakini alisema alikuwa ameniona. Kama Mungu atamfunulia mtu huyo, jambo fulani analojua, kama vile tu Filipino alivyoenda na kumchukua Nathanaeli na kumleta, wangapi watasema, “Italisuluhisha milele, kwangu mimi?”

182 Waweza kuinua mkono wako, kwamba sikujui. Inua tu mikono yako kama sikujui, sijui lolote kukuhusu. Sijui lolote kukuhusu, sijawahi kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi.

183 Sasa, kama Mungu atajalia hili, ni wangapi watasema, “Nitamkubali sasa hivi kama Bwana aliyefufuka, kama mponyaji wangu?”

184 Kukuponya, nisingeweza, bwana. Sina uwezo wa kuponya. Kitu pekee nilicho nacho ni karama ambayo Mungu ananiruhusu kufanya.

185 Na sasa nikiwa nimechoka na ni dhaifu, maono haya nusura yanie. Ni mabaya zaidi, ni magumu kuliko kuhubiri, au kusimama kwenye dimbwi. Ni magumu. Lakini Mungu ni mwema.

186 Unasumbuliwa na tatizo kwenye mgongo. Na hiyo ni uvimbe, wanakwambia, kwenye mgongo wako. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa utaamini?

187 Sasa tazama. Kadiri ningezungumza na huyu mtu, ndivyo mengi yangesemwa. Ninataka kukuuliza sasa, uwe na kicho tu. Uwe na kicho. Mwombee mtu fulani, uone kama Bwana atayafunua. Nitamwomba yeyote kati yenu kufanya jambo lile lile, liweke tu mawazoni mwako.

188 Mbona, mnaona, hamna kitu ndani yangu. Nisingeweza kukusaidia. Mimi ni mwanadamu.

189 Na, lakini Yesu ni Mungu, Naye yupo. Hivi huwezi. . . Je, macho yako yamefunguliwa ku—kuona hilo? Si unaangalia nyuma ya pazia, kuona? Kwa muda wa miaka elfu mbili, amekuwa hapa; amezungumza nanyi, katika Neno;

amezungumza nanyi, katika mahubiri yenu, wakati wote. Naye huyu hapa sasa, akijidhihirisha Mwenyewe.

¹⁹⁰ Ninajaribu kuwashikilia moyoni mwangu. [Ndugu huyo anasema, “Mgongo wangu unanisumbua.”—Mh.] Naam, naona umechunguzwa. Uko kwenye mgongo wako. Ni uvimbe. Nawe unamwomba mkeo. Kama Mungu atanionyesha tatizo la mkeo, je, utaniamini kama nabii Wake? Ni masikio yake. Isitoshe, bali naona kijana mwanamume akitokea. Huyu ni mwanao. Kama Mungu atanifunulia tatizo la mwanao, je, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Je, kusanyiko litaamini? Mvulana, hapa, ni ugonjwa wa fadhaa na ugonjwa wa ngozi. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Je, unaamini unapokea unachoomba? [Ndugu huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Basi nenda zako ukishangilia.

¹⁹¹ Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote?

¹⁹² Sasa nawatakeni mnifanyie jambo fulani. Wekeaneni mikono, kwa dakika moja tu. Popote tu mnaposimama, wekeaneni mikono.

¹⁹³ Ni wakati wa jinsi gani! Je, hamwezi kuona, enyi marafiki? Hamwezi kuelewa kuwa huyu hawezi kuwa ni mimi?

¹⁹⁴ Naam, maskini huyo mama yuko hapo amevaa miwani, akiwa na shida hiyo ya kike, usaha huo. Usijali kuuhusu, tena, ukiketi hapo. Umekwisha. Inageuka kuwa Nuru. Imeondoka kwako.

¹⁹⁵ Kitu Fulani kipo; kitu Fulani ambacho ni cha kimbinguni, kitu Fulani ambacho ni halisi. Anajua dhambi zako. Anajua yote kukuhusu. Je, yeye si ni Bwana Yesu? Basi, ninawaambia. Kama nimewaambia jambo hilo kuwa ni Kweli, Naye amelithibitisha kuwa ni Kweli, ninawaambia ukweli sasa. Kila mmoja wenu anaweza kuponywa sasa hivi, kama mtalikubali tu; sio kutoka kichwani mwako, bali kutoka moyoni mwako. Kama utalitatu sasa, ya kwamba uko Mbele ya Mungu mweza-yote, kwamba Yeye yuko sasa, hakuna haja ya mtu dhaifu kutoka nje ya jengo hili. Kila mmoja wetu anaweza kutoka mzima kabisa, ikiwa mtaamini tu. Kama akisikia maombi yangu hapa, atayasikia maombi yangu huko nje. Yeye si kwamba tu atayasikia maombi yangu, Yeye atasikia maombi yako.

¹⁹⁶ Sasa, Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Amethibitisha hilo. Biblia ilisema, “Amefufuka katika wafu.” Amethibitisha hilo. Je, hiyo ni kweli?

¹⁹⁷ Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Yesu alisema haya, Maneno Yake ya mwisho kabla hajaondoka duniani, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ni waaminio wangapi humu ndani? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wewe ndiye mwaminio sasa. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata

afya.” Je, ahadi hiyo ni ya kweli? Vema, ninyi ni waaminio. Mmewekeana mikono. Basi, Biblia ni ya kweli.

¹⁹⁸ Sasa kila mmoja wenu amwombee mwenzake, jinsi tu mnavyofanya kanisani mwenu. Wekeaneni mikono, kila mmoja amwombee mwenzake, mnapowekeana mikono sasa. Ombeaneni tu, ninapoomba sasa.

¹⁹⁹ Ee Bwana, kama ukija usiku wa leo na kulipokea Kanisa Lako, hatuna udhuru. Wewe uko hapa. Na huku picha hii ikining’inia ukutani, ya ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, Wewe ungali ni Mungu yeye yule usiku wa leo, pamoja na nguvu zile zile na madhihirisho yale yale. Umefufuka katika wafu, na hili ndilo thibitisho kwamba umefufuka katika wafu. Sasa, Bwana Mungu, fanya kazi kubwa mioyoni mwa watu. Samehe kila dhambi, na uponye kila ugonjwa. Jibu maombi yao, Bwana. Na sasa sikia maombi ya mtumishi Wako.

²⁰⁰ Sasa ninalaani kila ugonjwa, kila pepo, kila nguvu za ibilisi; na kumwambia ibilisi, “Ondoka kwa watu hawa. Waondokee, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Waache watu hawa. Wamewekeana mikono. Ni watumishi wa Mungu. Toka, Shetani. Ninakuapisha, katika Jina la Yesu. Toka, na utupwe gizani, wala usiwasumbue tena. Katika Jina la Yesu Kristo.”

²⁰¹ Ni wangapi wenu mnaamini Mungu amewaponya sasa hivi? Simameni kwa miguu yenu. Kama wewe ni kiwete, simama kwa vyovyote vile. Ndivyo hivyo. Hivi mimi sikuwaambia, mtauona utukufu wa Mungu? Kama kuna viwete wowote humu ndani ambao hawangeweza kutembea, tembeeni huku na huku kwenye marefu ya kanisa. Ikiwa kuna mtu yeyote hapa ambaye alikuwa kiziwi katika sikio moja, weka kidole chako kwenye sikio lililo zima na usikie kutoka kwa lililo bovu. Mtu yeyote hapa ambaye alikuwa akiteseka, hangeweza kuinua mkono wake; uinue. Kristo... Angalieni—angalieni mikono inayoinuliwa, waliokuwa wakiteseka mikononi mwao. Amina. Nilisema Yeye yuko hapa.

²⁰² Vema, Dada Gertie.

Yu hai, Yu hai, Kristo Yesu yu hai leo!
Anatembea nami na kuzungumza nami katika njia nyembamba ya maisha.
Yu hai, Yu hai, apate kutoa wokovu!
Unaniuliza ninajuaje Yeye yu hai? Yeye anaishi ndani ya moyo wangu.

²⁰³ Tena, kila mtu!

Yu hai, Yu hai, Kristo Yesu yu hai leo!
Anatembea nami, anazungumza nami katika njia nyembamba ya maisha.
Yu hai, Yu hai, apate kutoa wokovu!
Unaniuliza ninajuaje Yu hai? Yeye anaishi ndani ya moyo wangu.

204 Hebu kusanyiko hili kuu liseme, “Haleluya!” [Kusanyiko linasema, “Haleluya!”—Mh.] Bwana yu hai! “Bwana yu hai!” Lisifuni Jina Lake! “Lisifuni Jina Lake!” Haleluya! “Haleluya!”

Yu hai, Yu hai,

Hebu tumpungie mikono yetu.

. . . Yesu yu hai leo!

Anatembea nami, anazungumza nami katika njia nyembamba ya maisha.

Yu hai, Yu hai, apate kutoa wokovu!

Unaniuliza ninajuaje Yu hai? Yeye anaishi ndani ya moyo wangu.

205 Ni wangapi wanapenda wimbo huo wa zamani, semeni, “Amina!” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Peana mikono na mtu aliye karibu nawe. Useme, “Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!” Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!

Vema, *Imani Yangu Inakutegemea Wewe*. Loo, ni aja- . . .

. . . imani inakutegemea Wewe,
Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Nisikie sasa ninapoomba,
Ondoa hatia yangu yote,
Ee niruhusu tangu leo hii
Niwe Wako kabisa!

206 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kwa uchaji, katika Uwepo wa Mwenyezi Mungu. Bwana Mungu ampe baraka Zake kila mmoja. Bwana na awabariki, kila mmoja, kwa wingi, awape kilicho bora zaidi kilichopo. Neema Yake na ikae juu yenu, kila mtu akiinuka kwa ajili ya uponyaji wake. Usiukatae kamwe. Wengi wameokolewa. Wengi walimkubali Kristo. Kristo akifunua siri za moyo.

207 Tunawaalika tena, wageni, kwenye maskani yetu, kwenye ibada yetu.

208 Niliimba kwa muda kidogo tu, ili upako uniache kwa dakika moja, ili niweze kunena. Nina furaha ulikuwa hapa. Imekuwa siku nzuri kuwa pamoja nanyi. Mungu awabariki.

209 Kwa maskani, Jumapili ijayo usiku ni ushirika, kutawadha miguu. Yeyote kati yenu nyinyi watu katika ujirani wetu, simameni mtuone. Tuombeeni hata tutakapokutana tena.

210 Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa. Tutamwomba mchungaji, aje aturuhusu tufumukane, au aseme anachotaka.



58-0406E Ushahidi Wa Ufufuo
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org